MAISHA

# Usipomchanja mbwa wako faini Sh10 milioni

Hadija Jumanne, Mwananchi
hjumanne@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Zena Ayoub, anayeishi Kitunda Mwanagati jijini Dar es Salaam anasema aliwahi kuhama nyumba aliyokuwa anaishi na akasamehe kodi yake kutokana na kuwa mbwa wengi waliomtisha.

"Kuna siku nimekaa kibarazani akaja mbwa kwa kasi akawa kama anataka kunirukia, nikapiga kelele, akasimama. Mwenye nyumba akatoka na kumfukuza. Kuanzia siku hiyo nikawa naishi bila raha, hivyo nikaondoka na kusamehe kodi yangu ya miezi mitatu," anasema Zena.

Zena na watu wengine wengi wanaoogopa mbwa, wanatishwa na madhara ya kung'atwa na mnyama huyo kisha wauguze vidonda hata kuwa kwenye hatari ya kuambukizwa magonjwa.

Kila Septemba 28 dunia huadhimisha Siku ya Kichaa cha Mbwa ambao takwimu za Shirika la Afya Duniani zinaonyesha husababisha takriban vifo 70,000 kila mwaka.

Mganga Mkuu wa Serikali, Dk Aifello Sichalwe anasema watu 15,339 wameripoti kung'atwa na mbwa nchini kati ya Januari hadi Agosti 2022. Idadi hiyo imepungua kutoka matukio 39,787 yaliyorekodiwa kipindi kama hicho mwaka 2021.

"Takwimu hizi ni kutoka kwa watu walioripoti kwenye vituo vyote vya kutolea huduma, kuna waathirika ambao hawajifika katika vituo hivyo. Utafiti uliowahi kufanywa nchini mwaka 2002 ulikadiria vifo 1,499 husababishwa na kichaa cha mbwa," anasema Dk Sichalwe.

Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk Hezron Nonga anasema kwa wastani watu 3,387 hung'atwa na mbwa kila mwaka nchini, hivyo kuwa kwenye hatari ya kuambukizwa, kichaa cha mbwa kinachoenezwa pia na mbwa mwitu, paka, fisi na popo.

Mbwa na paka wanaozurura ovyo, anasema ndio waenezaji wakubwa wa kichaa cha mbwa na binadamu anaweza kuambukizwa kwa kugusa mate ya mnyama aliyeathirika, kupitia jeraha, mchubuko, jicho, pua au mdomo, ukiacha kung'atwa naye.

Ili kudhibiti uwezekano wa kusambaa kwa ugonjwa huo kwa binadamu, Dk Nonga anasema sheria inasema ukiamua kufuga mbwa, basi mfungie ili asizurure mtaani anakoweza kusababisha madhara na unatakiwa kumchanja.

"Kanuni ya uchanjaji wa mifugo ya mwaka 2020 inamlazimu kila mfuga mbwa au paka kumchanja ili kuzuia kichaa cha mbwa na endapo hatozingatia basi adhabu yake ni faini ya kati ya Sh500,000 hadi Sh10 milioni au kifungo cha mwaka mmoja jela," anasema Profesa Nonga.

Kumwacha mbwa au paka bila udhibiti, anasema ni kuvunja Sheria ya Serikali za Mitaa ya Mjini na Vijijini ya mwaka 1982 inayozuia mifugo kuzurura na unaweza kutozwa faini ya Sh50,000 hadi Sh300,000 au kifungo cha miezi sita jela au adhabu zote mbili.

Takwimu zinaonyesha Tanzania inao mbwa zaidi ya milioni 4.5 na asilimia 98 ni wa kienyeji ambao wanaachiwa wazurure mtaani. Mbwa hao ni wanaofugwa mjini na wale wa vijijini, hasa katika jamii za wafugaji ambazo huwatumia kuimarisha ulinzi wa mifugo.

Mkoa yenye idadi kubwa ya mbwa ni Arusha, Morogoro, Iringa, Tabora na mikoa yote ya kanda ya ziwa ambako kuna wafugaji wengi.

"Lakini matukio mengi ya kichaa cha mbwa yapo katika maeneo yanayopakana na hifadhi za wanyamapori kutokana na mwingiliano na binadamu," anasema.

### Mbwa mwenye kichaa

Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi ya Madaktari Wanaotibu Wanyama Wadogo Tanzania (Tasavo), Dk Sinare Sinare anasema kuna aina mbili za kichaa cha mbwa. Kwanza ni kichaa bubu ambacho mishipa ya mbwa hutulia kisha hupooza na kufa ndani ya siku nne. Na aina ya pili ni mbwa kuwa na hasira ambacho humchukua siku kumi kupoteza maisha.

"Mbwa mwenye kichaa huwa mkali, hutoa mate kwa sababu hawezi kumeza, mishipa ya koromeo hufunga na hung'ata watu ovyo. Wakati mwingine anauma miti au mbwa wenzake," anasema Dk Sinare.

Dalili nyingine, Dk Nonga anasema ni mbwa kuchanganyikiwa na kutoa ulimi na meno nje. Anasema huchukua siku 10 hadi miezi sita kuonyesha dalili za ugonjwa tangu mbwa anapoambukizwa.

"Baada ya kuambukizwa mbwa hukaa muda fulani na hupooza miguu ya nyuma na hivyo hutembea kwa kujiburuza kiuno kwa sababu hawezi kusimama," anasema Dk Nonga.

"Tahadhari muhimu kwa jamii kuizingatia ni kuepuka kumchokoza au kumpiga mbwa anayepita barabarani kwani anaweza kukung'ata"

Dk Hezron Nonga

**Mil 4.5**

Makadirio ya idadi ya mbwa waliopo Tanzania.

**60,000**

Idadi ya mbwa wanaotarajiwa kuchanjwa mwaka huu hapa nchini.



Ofisa Mifugo, Mbise Baraka, akimchunguza mbwa kabla ya kuanza kumpatia matibabu. **Picha na Hadija Jumanne**



Maofisa mifugo, Mbise Baraka (kushoto) na Mswao Raphael wakimshona mbwa aliyejeruhiwa baada ya kupigwa na wenzake akiwa bandani eneo la Darajani Kigamboni, jijini Dar es Salaam.

### Huduma kwa aliyeng'atwa

Ofisa mifugo wa taasisi ya ustawi wa wanyama Tanzania (Taweso), Mbise Baraka anasema endapo mtu atang'atwa na mbwa au mnyama mwingine yeyote, alioshe jeraha kwa maji mengi yanayotiririka na sabuni kwa angalau dakika 15 kisha apake iodine halafu akimbizwe hospitali.

Dalili zinazojitokeza ni mtu kupata homa, maumivu ya kichwa na viungo, muwasho sehemu ya jeraha, kuogopa mwanga au kuogopa kunywa maji, kukosa hamu ya kula, kukosa usingizi, kichefuchefu na kutapika.

Dalili nyingine ni kuanza kubweka kama mbwa, kutiririkwa mate ovyo, kuchanganyikiwa, kupiga vitu ovyo, kuweweseka au kushtuka mara kwa mara hata kupoteza fahamu, kupooza, kudhoofu mpaka kufa kabisa.

Kasi ya kusafiri kwa virusi wa kichaa cha mbwa mwilini, Dk Sinare anasema hufuata mkondo wa neva za fahamu kuelekea kwenye uti wa mgongo na vikifika huelekea kwenye ubongo.

"Ni vizuri mbwa aliyekung'ata awekwe chini ya uangalizi kwa siku 10, kama ana kichaa basi ataonyesha dalili zake," anasema Dk Sinare.

### Mikakati ya Serikali

Dk Sichalwe anasema kuwa wanaendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya madhara ya kichaa cha mbwa kwa sababu mtu akipata ugonjwa huo ni vigumu kupona, hivyo wanajikita kuzuia badala ya kutibu.

"Tunasimamia miongozo na sheria zilizopo kwa kuhakikisha jamii ya mbwa na paka wanapata chanjo ya kuzuia kichaa cha mbwa," anasema Dk Sichalwe.

Kwa upande wake, Dk Nonga anasema hamasa ya kuchanja mifugo hiyo imekuwa ikiongezeka kila mwaka. Kwa mwaka wa fedha 2021/22, anasema mbwa milioni 1.6 na paka 6,833 walichanjwa kuzuia kichaa cha mbwa.

Idadi hiyo iliongezeka kutoka mbwa 986,195 na paka 5,152. Katika mwaka huu wa fedha, anasema kati ya Julai na Septemba wameshachanja mbwa 323,638 na paka 28,933 kwenye halmashauri 101.

"Tahadhari muhimu kwa jamii kuizingatia ni kuepuka kumchokoza au kumpiga mbwa anayepita barabarani kwani anaweza kukung'ata," anashauri Profesa Nonga.

Ingawa dunia itaadhimisha Siku ya Kichaa cha Mbwa Septemba 28, Tanzania imetangaza wiki ya kuelimisha ugonjwa huo kuanzia Septemba 26 mpaka Oktoba 2 ila kilele cha maadhimisho hayo kinafanyika kitaifa leo jijini Dodoma kikihudhuriwa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki.

Katika maadhimisho haya yanayofanyika katika vituo vyote vya huduma za mifugo nchini, Dk Nonga anasema "tunatarajia kuchanja mbwa na paka 60,000."

CamScanner

UK 6.



## Wasio na uwezo bima ya afya kutambuliwa kupitia Tasaf

HABARI UK 2

SUPA JACKPOT
TZS. 1,034,905,195
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#

# MWANANCHI

TANZANIA


Jumatano, Septemba 28, 2022 MWANANCHI.CO.TZ ISSN 0856-7573 NA.8084 BEI: TSH 1,000, KSH 60

## Mkataba kodi mara 2 mjadala



**Dar es Salaam.** Baada ya Tanzania na Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) kutia saini makubaliano ya kuondoa utozaji kodi mara mbili, wataalamu wa kodi wameibuka na ... UK 2

## Vigezo ufadhili elimu vyatajwa



**Dodoma.** Serikali imetang masharti saba kwa wanafu watakaonufaika na ufadhili elimu kupitia mfuko wa Rais (Samia Scholarship), Ikiwer kuhakikisha ... UK 5

## Faini Sh10 milioni kutochanja mbwa



**Dar es Salaam.** Wakati watu 15,339 wakiripoti kung'atwa na mbwa nchini kati ya Januari hadi Agosti 2022, imeelezwa kuwa kitendo cha kumtomchanja mbwa wako kinaweza... UK 6

CamScanner

eme vijijini, mbazaji wa ... ziada, TREEP inatarajiwa ... na Co-TTL, Mbuso Gwafila.

HABARI LEO UK 2.

# * Makundi ya mifugo bado tishio Ihefu *

**Na Mwandishi Wetu, Mbarali**

HIFADHI ya Taifa ya Ruaha bado ina hali mbaya kutokana na makundi ya mifugo kuendelea kuchungwa ndani ya Bonde la Ihefu lenye ardhi oevu hivyo kuhatarisha uwepo wa Mto Ruaha Mkuu.

Uvamizi huo wa mifugo ndani ya hifadhi hiyo umesababisha uharibifu wa mazingira na hivyo kuiweka ikolojia ya hifadhi hiyo kuwa katika hatari ya kupotea.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk Selemani Jafo amefanya ziara katika eneo hilo kwa lengo la kuangalia uharibifu wa mazingira uliofanywa na wafugaji.

Amewataka wafugaji hao kuondoka kwa hiari.

Dk Jafo akiwa ameongozana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya na maofisa wa Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA), walitumia ndege maalumu kufanya ukaguzi katika bonde hilo ambako walishuhudia idadi kubwa ya mifugo.

Alisema mbali na mifugo hiyo kuonekana katika makundi makubwa, lakini pia wafugaji hao wamejenga mazizi pamoja na nyumba za kuishi ndani ya bonde hilo na hivyo kusababisha uharibifu mkubwa wa mazingira.

Alisema hali waliyoishuhudia ndani ya eneo hilo isipodhibitiwa mapema, Mto Ruaha Mkuu unaweza ukapotea kabisa na kusababisha miradi ya maendeleo inayotegemea mto huo ukiwamo Mradi wa Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere kukwama.

"Nimeshuhudia kabisa sasa hivi hakuna maji ambayo yanapita kwenye eneo hilo kutiririka kwenda Mto Ruaha, hapa nimeambiwa kwamba eneo hili ndio chanzo kikuu cha huu mto, sasa kama hali ndivyo ilivyo kuna hatari kubwa mto huu ukakauka kabisa," alisema Dk Jafo.

Alisema viongozi wakuu wa nchi wameelekeza mazingira kuhifadhiwa ikiwemo chanzo cha Mto Ruaha na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na kwamba aliamua kwenda kufanya ziara hiyo baada ya kuona baadhi ya picha kwenye mitandao ya kijamii na vyombo vya habari.

Aliwapongeza viongozi wa Mkoa wa Mbeya na wa Tanapa kwa kuanzisha operesheni maalumu ya kuiondoa mifugo hiyo na kwamba operesheni hiyo inatakiwa iendelee mpaka wahakikishe mifugo yote imeondolewa.

Mkuu wa Hifadhi ya Ruaha, Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi, Godwell Ole Meng'ataki alisema kwa sasa wanaendelea na operesheni ya kuiondoa mifugo hiyo ambayo walianza kuitekeleza Septemba 13, mwaka huu.

Alisema katika kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Julai 2021 mpaka sasa wamekamata mifugo zaidi ya 16,000 katika matukio 60 na kwamba zaidi ya wafugaji 190 walikamatwa na kuchukuliwa hatua mbalimbali za kisheria.

Ole Meng'ataki alisema katika kipindi hicho cha mwaka mmoja wamekusanya zaidi ya Sh bilioni 1.6 ambazo zinatokana na faini wanazotozwa wafugaji hao.

"Tunawatoza shilingi 100,000 kwa kila mfugo unaokamatwa, lakini uzoefu tulionao ni kwamba wafugaji hawa wamekuwa jeuri sana, unaweza ukakamata mifugo hata 800 kwa siku, lakini kufika kesho yake wanakuwa wamelipa faini na wanakuja kuchukua mifugo yao," alisema Ole Meng'ataki.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alisema idadi ya mifugo iliyoko ndani ya bonde hilo ni mingi kuliko hata wanyamapori walioko ndani ya hifadhi hiyo jambo ambalo linahatarisha uwepo wa hifadhi hiyo.

na Mwakilishi wa Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF, Oscar Maduhu (wakwanza kushoto) wakati wa ziara ya kikazi ya Naibu Waziri huyo iliyolenga kukagua mradi wa ujenzi wa bweni la wanafunzi katika shule ya Sekondari Bukundi wilayani Meatu. Wa kwanza kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Meatu, Fauzia Ngatumbura. (Picha na Ofisi ya Rais Utumishi)

Salaam kwa ajili ya kuonesha heshima kwa Mtume Muhammad (SAW).

HABARI LEO UK 7.

# 'Watoto wanaopewa maziwa hufanya vizuri darasani'

**Na Sifa Lubasi**

MSAJILI wa Bodi ya Maziwa Tanzania (TDB), Dk George Msalya amesema tafiti zilizofanyika zinaonesha watoto wanaopewa maziwa wanafanya vizuri katika masomo yao kulinganisha na wasiopata maziwa.

Akizungumza wakati wa maadhimisho ya kitaifa ya siku ya kunywa maziwa shuleni yaliyofanyika katika Shule ya Dodoma Viziwi, Dk Msalya alisema kuwapa watoto maziwa kunawajenga vizuri kiakili.

"Tafiti zimefanyika, watoto wanaopewa maziwa wanafanya vizuri katika masomo yao kuliko wale wasiopata maziwa," alisema.

Alisema Tanzania huzalisha lita bilioni 3.4 za maziwa kwa mwaka na kwamba ni kiasi kidogo cha maziwa ambacho huagizwa kutoka nje ya nchi. "Maziwa ni chakula cha msingi sana cha watoto na watu wazima pia," alisema Msalya.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Dodoma Viziwi, Kennedy Maingu alisema shule hiyo kwa mwezi wa Septemba wanafunzi walikuwa wakipata maziwa na kwamba kumekuwa na mabadiliko katika afya zao na maendeleo kwenye masomo.

Maingu alisema Bodi ya Maziwa Tanzania ilihudumia na kuwezesha wanafunzi kupata maziwa shuleni kwa mwezi wote wa Septemba na kuwataka wadau wengine kujitokeza kusaidia wanafunzi kupata maziwa shuleni.

Ofisa Lishe kutoka Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), Stella Kimambo alisema FAO na Serikali ya Tanzania kupitia programu inayofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU) inayoitwa AGRI-CONNECT zimezindua kampeni ya kitaifa ya lishe ili kujenga tabia zinazofaa za mlo kwa kutumia vyakula vinavyopatikana nchini.

Kimambo alisema maadhimisho hayo yanalenga kufikisha ujumbe kwa jamii iweze kutumia maziwa kwa ajili ya kuimarisha afya.

"Badala ya mtoto kula ice cream au ubuyu wa rangi, anywe glasi moja ya maziwa," alisema na kuongeza kwamba glasi moja ya maziwa inaweza kuleta mabadiliko makubwa kwenye afya yam toto na kwamba si lazima mtu anywe maziwa ya ng'ombe bali hata maziwa ya soya.

Maadhimisho hayo yalienda sambamba na ugawaji wa maziwa kwenye shule zenye wanafunzi wenye mahitaji maalumu za Nkuhungu, Chinangali, Mlezi na Dodoma Viziwi.

Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri wa Bodi ya Maziwa, Zacharia Masanjiwa alisema unywaji maziwa shuleni unatakiwa kuwa endelevu ili kuboresha afya na akili za watoto.

Kaimu Meneja Masoko wa Bodi ya Maziwa Tanzania, Joseph Semu alisema Shirika la Afya Duniani (WHO) linasema wastani wa unywaji maziwa ni lita 200 kwa mwaka lakini hapa nchini wastani uko chini wa lita 62 kwa mwaka.

CamScanner

na vinatumika.

rimu Sh bilioni 920.175.

Haya yamebainishwa jijini

huo kwa niaba ya waziri mkuu, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais

utoaji wa huduma za ustawi wa jamii nchini.

HABARI LEO UK 14.

# * Wafugaji wakumbushwa utamaduni wa kuhifadhi malisho

**Na Sifa Lubasi**

WAFUGAJI nchini wametakiwa kuwa na utamaduni wa kuhifadhi malisho ili kuweza kukabiliana na ukame mkubwa unaotishia kuua mifugo mingi na kusababisha hasara kubwa kwao.

Kauli hiyo imetolewa juzi na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Idara ya Mifugo, Tixon Nzunda wakati wa ziara ya kutembelea Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (TARILI) na Taasisi ya Wakala wa Mafunzo ya Mifugo (LITA), kampasi ya Mpwapwa.

Nzunda aliwataka wafugaji kuwa na utamaduni wa kuhifadhi malisho.

Pia amezitaka Taasisi zote za utafiti wa mifugo hapa nchini kuongeza kasi ya uzalishaji na uvunaji wa majani ambayo yatauzwa kwa wananchi ili kuweza kutunza mifugo yao na kupata tija katika ufugaji wao.

Akizungumzia mradi wa uzalishaji wa ndama kwa kutumia viini tete alisema wakati serikali inajipanga kuondoa changamoto zilizopo lazima kuanza kufanya kile kinachowezekana kufanyika kwa kutumia rasilimali zilizopo.

Kwa upande wake, Mtaalamu wa kitengo cha maabara ya uzalishaji kwa kutumia viini tete, Kabun Thomas alisema tayari wamefanikiwa kuzalisha ndama mmoja ambaye ametokana na viini tete.

Hata hivyo, alisema kuwa ili kukamilisha vifaa vyote vilivyobaki taasisi hiyo inahitaji jumla ya Sh milioni 800 ili kuweza kuvuna, kugandisha na kuhifadhi viini tete.

Akikagua mradi wa ujenzi wa bweni la Taasisi ya LITA, Nzunda aliwataka viongozi wa tasisi hiyo kuongeza kasi katika umaliziaji wa bweni hilo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi mkuu wa Taliri, Profesa Erick Komba aliwataka watumishi wote wa Taliri nchini kufanya tafiti zinazolenga kuleta mabadiliko makubwa kwa jamii hususani wafugaji na wavuvi.





# Mifugo inavyohatarisha uhai wa ikolojia ya Bonde la Ihefu

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

HALI ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha bado ni tete kutokana na makundi ya mifugo kuendelea kuchungwa ndani ya Bonde la Ihefu lenye ardhi oevu ambalo lipo ndani ya hifadhi hiyo.

Uvamizi huo pia umesababisha uharibifu wa mazingira ndani ya hifadhi, hivyo kuiweka ikolojia ya hifadhi hiyo kuwa katika hatari ya kupotea.

Juzi Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Selemani Jafo alifanya ziara katika eneo hilo kwa lengo la kuangalia uharibifu wa mazingira uliofanywa na wafugaji, aliwataka wafugaji hao kuondoka kwa hiari.

Katika ziara hiyo, Waziri Jafo akiwa ameongozana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya na maofisa wa Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA), walitumia ndege maalumu kufanya ukaguzi katika bonde hilo, walishuhudia idadi kubwa ya mifugo.

Waziri Jafo alisema mbali na mifugo hiyo kuonekana katika makundi makubwa lakini wafugaji hao wamejenga mazizi pamoja na nyumba za kuishi ndani ya bonde hilo, hivyo kusababisha uharibifu mkubwa wa mazingira.

**Idadi ya mifugo iliyoko ndani ya bonde hilo ni mingi kuliko hata wanyamapori walioko ndani ya hifadhi hiyo jambo ambalo linahatarisha uwepo wa hifadhi hiyo.**

Alisema hali waliyoishuhudia ndani ya eneo hilo isipodhibitiwa mapema Mto Ruaha Mkuu unaweza ukapotea na kusababisha miradi ya maendeleo inayotegemea mto huo ukiwamo Mradi wa Bwawa la kuzalisha Umeme la Nyerere kukwama.

Alisisitiza kwamba viongozi wakuu wa nchi wameelekeza mazingira kuhifadhiwa ikiwamo chanzo cha Mto Ruaha na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na kwamba aliamua kwenda kufanya ziara hiyo baada ya kuona baadhi ya picha kwenye mitandao ya kijamii na vyombo vya habari.

Jafo aliwapongeza viongozi wa Mkoa wa Mbeya na wa TANAPA kwa kuanzisha operesheni maalumu ya kuiondoa mifugo hiyo na kwamba operesheni hiyo inatakiwa iendelee mpaka wahakikishe mifugo yote imeondolewa.

Mkuu wa Hifadhi ya Ruaha, Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi, Godwell Ole Meng'ataki, alisema kwa sasa wanaendelea na operesheni ya kuiondoa mifugo hiyo ambayo walianza tangu Septemba 13, mwaka huu.

Alisema katika kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Julai 2021 mpaka sasa wamekamata mifugo zaidi ya 16,000 katika matukio 60 na kwamba zaidi ya wafugaji 190 walikamatwa na kuchukuliwa hatua mbalimbali za kisheria.

Ole Meng'ataki alisema katika kipindi hicho cha mwaka mmoja wamekusanya zaidi ya Sh. bilioni 1.6 ambazo zinatokana na faini ambazo wafugaji hao wamekuwa wakitozwa.

"Tunawatoza Sh. 100,000 kwa kila mfugo unaokamatwa lakini uzoefu tulionao ni kwamba wafugaji hawa wamekuwa jeuri sana, unaweza ukakamata mifugo hata 800 kwa siku lakini kufika kesho yake wanakuwa wamelipa faini na wanakuja kuchukua mifugo yao," alisema Ole Meng'ataki.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema idadi ya mifugo iliyoko ndani ya bonde hilo ni mingi kuliko hata wanyamapori walioko ndani ya hifadhi hiyo jambo ambalo linahatarisha uwepo wa hifadhi hiyo.

Alisema askari wa TANAPA wanaofanya operesheni ya kuondoa mifugo hiyo wanafanya kazi katika mazingira magumu kwa maelezo kuwa wanaswaga umbali wa zaidi ya kilomita 50 kutoka hifadhini mpaka kwenye kambi ya Ikoga Mpya.

Hata hivyo Waziri Jafo aliahidi kurejea katika eneo hilo na mawaziri wenzake wanaohusika na masuala mbalimbali kwa ajili ya kujadiliana namna sahihi ya kuiondoa mifugo hiyo.

CamScanner